
# 19 MAONO JUU YA ULIMWENGU ULIO BORA ZAIDI



Je, hili ndilo kusudi la Mungu kutuacha sisi katika ulimwengu huu wa mateso?

Kwa wengi, maisha yamegeuka na kuwa jinamizi,

- kwa kadiri wanavyoteseka kwa magonjwa,
- wamejawa na maumivu; kushindania chakula;
- kutoelewana majumbani;
- kukwazwa na wapendwa wao;
- kufanywa watumwa wa kazi.
- Kwa ajili ya sababu nyingine nyingi, maisha yamekuwa ni mzigo mzito.

Je, ni ndoto ngapi ambazo hazikuweza kutimilika!

- Wengi wanapotafuta urafiki na kuishia kwenye kukataliwa.
- Wengine wanatamani kuwa na afya lakini badala yake wanasumbuka na ugonjwa.
- Wengine wanatamani kuwa na makao yao wenyewe, lakini inaonekana kwamba haiwezekani.
- Nasi sote tunatamani kama wapendwa wetu wangekuwa karibu nasi wale ambao kifo kimewaondoa kutoka kwetu.

**1. Mungu ametuahidi makao yasiyo na uvuli. Je, ni lini tutakapoyapokea? Yohana 14:1-3.**

______________________________________________________________________

- Tutapewa dunia mpya kama ile waliyopewa wazazi wetu wa kwanza (Mwanzo 1:31). Kila kitu kitakuwa ni kizuri ikijumlishwa na mimea, maua, pamoja na wanyama. Tutafurahia amani timilifu pamoja na furaha.
- Mwanadamu alipokea vipawa vinne pale alipoumbwa: uzima wa milele, tabia kamilifu, makao mazuri, utawala juu ya kila kitu.
- Dhambi ikaleta maumivu badala ya vipaji hivi vyote.

**2. Kusudi la kifo cha Kristo lilikuwa ni nini? 1 Yohana 2:25.**

______________________________________________________________________

- Kwa njia ya Kristo tutaweza kuwa huru kutokana na utumwa wa yule mwovu, na ndani Yake Yeye mambo yote yatakuwa mapya. Isaya 45:22.

## *MBINGU MPYA NA NCHI MPYA ZITAKUWA KAMA NINI?*

**3. Hivi sasa kuna mbingu ngapi, kwa kulingana na Biblia? 2 Wakorintho 12:2-4.**

______________________________________________________________________

- Mbingu ya kwanza ni anga linayoizunguka dunia-hewa.
- Mbingu ya pili ni anga-anga la nyota (Zaburi 19:1).
- Mbingu ya tatu ni kile kiti cha enzi cha Mungu (1 Wafalme 8:30).

**4. Je, Mungu ametuandalia nini? 1 Wakorintho 2:9.**

______________________________________________________________________

5. **Pale walipotafakari juu ya maskani ya mbinguni kwa jicho la imani, waumini hawa wa kale walisema nini pale walipotafakari maisha yao ya hapa duniani? Waebrania 11:13-16.**

______________________________________________________________________

6. **Ile nchi mpya itakuwaje? Isaya 35:1, 2, 6 (sehemu ya pili), 7.**
   - *Hakutakuwako na majangwa mapana ama bahari kubwa sana.*
   - *Dunia nzima itakuwa ni bustani yenye uzuri wa kushangaza (Isaya 55:13).*
   - *Mauwa mazuri zaidi kuliko mauwa mazuri zaidi tunayoyafahamu (Ufunuo 22:2).*
   - *Matunda mazuri ambayo hapana mwanadamu ye yote aliyepata kuyajaribu hapa.*
   - *Kijani kibichi kilichokolea sana kuliko kijani ya chemchemi.*
   - *Kutakuwako na mito, vijito na maziwa yenye kuangaza kama kioo.*

7. **Je, unabii unasemaje juu ya masikilizano katika jamii ya wanyama? Isaya 11:6-9; 32:17, 18.**

______________________________________________________________________

8. **Je, ni kitu gani ambacho hakitakuwako kule? Isaya 33:24; 35:3-6.**

______________________________________________________________________

9. **Je, kutakuwa na nini badala ya huzuni? Isaya 35:9, 10; 65:17-25.**

______________________________________________________________________

10. **Je, tutafanya kazi ama tutakaa kizembe? Isaya 65:21-23.**

______________________________________________________________________

11. **Yerusalemu Mpya, ule mji mkuu, utakuwaje? Ufunuo 21:1-5, 10-12.**
    - a) *Kipimo chake "furlong" (1/8 ya maili) 12,000 (mstari 16), ama km 2,200.*
    - b) *Umejengwa kwa ________________________, sawa na kioo kinachoangaza (mstari 18).*
    - c) *Ukuta wake una misingi __________________ iliyojengwa kwa mawe ya thamani (mstari 19, 20).*
    - d) *Milango 12 iliyofanywa kwa lulu kubwa kubwa (mstari 21).*
    - e) *Hakutakuwako na usiku kwa sababu Kristo atakuwa ndio nuru yao (mstari 23).*
    - f) *Kutokea katika kile kiti cha enzi cha Mungu kutakuwako na mto wenye maji yenye kuangaza kama kioo yakitiririka na katika kila upande wa mto kuna ule mti wa uzima (Ufunuo 22:1, 2).*
    - g) *Tutakuwa pamoja na Yesu kwa milele (mstari 3, 4).*

12. **Je, ni katika siku gani ambapo tutakusanyika ili kumwabudu Mungu? Isaya 66:22, 23.**

______________________________________________________________________

13. **Je, twawezaje kufahamu kwamba ahadi hizi zote ni za kweli?**
    - Uzitumainie ahadi za Mungu. Hatuzungumzi juu ya mambo ya kubuniwa ama kuwaziwa tu, bali ni juu ya ahadi za Mungu wa upendo.
    - a) Matabirio 2,300 ambayo yanatimilika mbele ya macho yetu ndio dhamana ya kwamba Mungu wala hasemi uongo.
    - b) Ile kafara pale Kalvari isingekuwa na maana iwapo neno hili lisingekuwa ni kweli.
    - c) Pale Kristo ajapo; tutabadilishwa na kuwa viumbe tusiopatwa na umauti (1 Wakorintho 15:51-58).

## *NAWEZAJE KUPATA NAFASI MBINGUNI?*

**14. Je, ni kitu gani ambacho napasa kukifanya kwa nafasi ya kwanza? Matendo 16:31.**

________________________________________________________________

*Umpokee Kristo, kwa njia ya imani, kama Mwokozi wa nafsi yangu na Bwana wa maisha yangu.*

**15. Je, nifanye nini ili nipate uzima wa milele? Yesu alifundisha nini? Mathayo 19:17 (sehemu ya mwisho).**

________________________________________________________________

*a) Yeye ____________________ atayarithi haya yote (Ufunuo 21:7).*

*b) Hakutakuwako na nafasi kwa waasi kule; ni wale pekee ambao majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima ndio wataweza kufika mahali pale (Ufunuo 21:8, 27).*

*Ambapo neno hili ''tenda'' linapotumika, na iwe wazi kwamba hili silo chimbuko, bali ni matokeo ya wokovu. Ni sifa za Kristo pekee ndio msingi wa wokovu wetu. Kujitoa na kutii kwetu ni wajibu wetu juu ya upendo wa Mungu, Yeye ambaye tumemkubali sio tu kama Mwokozi bali pia kama Bwana wa maisha yetu.*

## *HITIMISHO:*

- Kristo alifanya sehemu Yake pale Kalvari. Yaliyosalia yanategemea juu yako. “Kama mkikubali, mtakula mema ya nchi” (Isaya 1:19).
- Huu sasa ndio wakati wa kufanya maamuzi na kushikamana na mwamba wa wokovu ambao ni Kristo Yesu.
- Kuupokea mwaliko wa Mungu hivi leo! (Waefeso 5:14-17).

***Uamuzi wangu:*** *Ninatamani kushiriki katika nchi iliyo bora.* ○ *Ndio* ○ *Hapana*